MARIE STOPES TANZANIA



# KUHAKIKISHA HAKI YA MAAMUZI KATIKA AFYA YA UZAZI

## MATOKEO YA MST YA NUSU MWAKA 2023

### Kupunguza pengo la upatikanaji huduma kupitia kuimarisha mfumo wa sekta ya afya ya umma

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2023, kupitia programu yetu ya kuimarisha sekta ya umma, tulifikia zaidi ya vituo vya umma 148 ambapo tuliwajengea uwezo watoa huduma ili waweze kutoa huduma kamili za uzazi wa mpango na huduma za baada ya mimba kuharibika, usimamizi wa ugavi, usimamizi wa takwimu, kuhakikisha ubora wa huduma, pamoja na kugawa vifaa tiba ili kuimarisha utoaji huduma kwa wateja, huku tukiweka mkazo katika huduma rafiki kwa vijana na watu wenye ulemavu.

### Kufikia wasiofikiwa na huduma za afya ya uzazi

Kupitia mkakati wetu wa kufikia jamii kupitia huduma za mkoba ambao huwezesha kuwafkia wateja wenye uhitaji mkubwa hasa vijana na watu walio katika mazingira magumu, tumeendelea kushirikiana kwa ukaribu na serikali katika kuboresha upatikanaji wa taarifa na huduma za uzazi wa mpango katika maeneo ya vijijini na yasiyofikiwa kwa urahisi nchini Tanzania.

### Afya ya Uzazi mikononi mwa mteja: Hatua muhimu katika kukidhi haja za wateja wa uzazi wa mpango

Marie Stopes Tanzania inatumia mkakati wa masoko jamii wenye lengo la kuongeza upatikanaji wa bidhaa muhimu za afya ya uzazi zilizosajiliwa na zenye ubora wa hali ya juu na bei nafuu kuhakikisha wateja wanazifikia na kuzitumia popote wawapo. Katika kipindi hiki, MST imeendelea kusambaza katika masoko kondomu za Lifeguard na vidonge vya misoclear ili kutumika katika kutoa huduma kwa wanawake mara baada ya mimba kuharibika na pia huduma za jumla za akina mama wakati wa kujifungua kupitia njia mpya na za zamani za usambazaji.

Ili kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za afya ya uzazi, kituo chetu cha huduma za simu ya bure kilichounganishwa na akaunti zetu katika mitandao ya kijamii kilipokea simu zipatazo 10,133 na kutoa rufaa na taarifa kwa wateja 1,666. Kikiendeshwa na wahudumu waliopatiwa mafunzo, kituo chetu kimeendela kuwa msaada na manufaa kwa wateja wenye uhitaji wa taarifa na huduma za afya hali ambayo imeendelea kujenga msingi wa kukidhi matakwa ya wateja, usalama na hatimaye matokeo chanya katika afya.

> "Ninajisikia Faraja kuwa miongoni mwa watu wanaohakikisha haki ya maamuzi binafsi kuhusu afya ya uzazi inafikiwa hasa kwa jamii zisizofikiwa kirahisi."
>
> **Amina,** Kiongozi wa Timu ya Huduma za Mkoba, Kilindi.

### Takwimu ya Matokeo Juni 2023

**838K**
Jumla la wateja waliofikiwa

**19.3%**
Ya wateja wote waliofikiwa ni chini ya miaka 20

**1.2M**
Mimba zisizotarajiwa zilizoepukwa

**281K**
Utoaji mimba usiosalama ulioepukwa

**1.5K**
Vifo vya akina mama vilivyoepukwa

**2.5M**
Alama za muda wa uzuiaji mimba zilizozalishwa

*Alama za muda wa kuzuia mimba ni kipimo kinachokadiria muda wa ulinzi wa kutokupata ujauzito unaopatikana baada ya kutumia njia za uzazi wa mpango katika kipindi cha mwaka mmoja.

# UCHECHEMUZI UNAOLENGA **HAKI ZA AFYA YA UZAZI** TANZANIA

Uchechemuzi uliofanywa na MST umechangia kupatikana kwa mabadiliko ya kisera, kikanuni na miongozo na sheria mbalimbali.

Katika nusu ya mwaka 2023, tulishirikiana na wadau wengine pamoja na Wizara ya Afya kuwezesha mapitio ya Mwongozo wa Jumbe za Uzazi wa Mpango kwa lengo la kuingiza mabadiliko yaliyojitokeza na uhitaji wa kuyapa kipaumbele maboresho ya ubora na taarifa sahihi juu ya uzazi wa mpango ili kuhakikisha upatikanaji wan jia mbalimbali za uzazi wa mpango.

Vilevile, MST imeshirikiana na wizara na wadau wengine kufanya mapitio ya Mwongozo wa Kitaifa wa Huduma za Mkoba za Afya ya Uzazi kuhakikisha ridhaa kwa wateja wa njia za uzazi wa mpango za muda mrefu. Hatua hii itahakikisha wateja wanapatiwa huduma ya unasihi kuhusu machaguo ya njia na usimamizi na ufuatiliaji wa matukio yenye madhara.

> "Kuwekeza katika muda, ubia na uwekezaji wa pamoja, tuna imani kuwa matokeo chanya yanaweza kupatikana. Tunapenda kuwashukuru kwa dhati kabisa, washirika na wafadhili wetu kwa kuunga kwao mkono jitihada za kuhakikisha utolewaji wa huduma jumuishi za afya ya uzazi leo na wakati ujao."




Kutana na **Nassoro,** mtoa huduma za Afya ya Uzazi wa serikali aliyejengewa uwezo kupitia Marie Stopes

## "Sasa nina ujasiri katika kutoa njia za uzazi wa mpango za muda mrefu"

Nassoro, afisa wa uuguzi, alianza kazi hii mwaka 2012 katika Hospitali ya Kinyonga, hospitali ya wilaya huko Kilwa, mkoani Lindi. Baadaye alirudi shule na kuhitimu mwaka 2018, na aliporudi, alihamishiwa Kituo cha Afya cha Masoko kilichopo Kilwa Masoko. Kama watoa huduma wengine wengi, anakiri hakuwahi kufundishwa kwa kina kuhusu kutoa huduma za uzazi wa mpango wakati akiwa masomoni.

"Elimu kidogo ya huduma za uzazi wa mpango niliipata kupitia utoaji wa huduma wakati wa mafunzo kwa vitendo. Tangu wakati huo, nilijenga shauku ya kutoa huduma za uzazi wa mpango na nilikuwa na hamu kubwa ya kufanya kazi katika kitengo cha Huduma za Afya ya Mama, Baba na Mtoto, kwa hiyo nilikuwa nikipenda kutafuta fursa za kujifunza wakati natoa huduma, hasa njia za muda mfupi.

Ingawa nilikuwa natoa huduma, nilikutana na changamoto kadhaa ikiwemo ukosefu wa taarifa na ujuzi mdogo niliokuwa nao havikuniruhusu kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa kujiamini kwa wateja niliowahudumia. Nilijua mambo machache sana kuhusu njia za uzazi wa mpango na sikuwa na uwezo wa kutoa ushauri wa kutosha kwa wateja ili kukidhi mahitaji yao ya uchaguzi wa njia za uzazi wa mpango.

Wakati fulani kituo chetu kiliingizwa katika mradi unaotekelezwa na Marie Stopes Tanzania, na nilipewa muuguzi aliyepatiwa mafunzo na mwenye uzoefu ambaye amekuwa akitutembelea mara kwa mara kutuongoza. Hii imeleta mabadiliko makubwa katika kazi yangu kama mtoa huduma za uzazi wa mpango. Sasa natoa huduma kwa ujasiri. Muuguzi anatupatia taarifa mpya na namna sahihi ya utoaji huduma na kutufundisha kuhusu utoaji huduma bora, kuweka kumbukumbu, na kuandaa na kutuma ripoti.

Tangu wakati huo, idadi ya wateja imeongezeka hasa kwa njia za muda mrefu. Katika kituo chetu, tunatoa huduma za uzazi wa mpango kwa takribani wateja 30 kwa siku. Idadi inaongezeka sana mwishoni mwa msimu wa mavuno kwani wengi wa wateja ni wakulima," anasema Nassoro.

Kama mnufaika, yeye pia anatumia utaalamu alioupata anajenga uwezo kwa watoa huduma wengine kituoni walio katika kitengo cha afya ya mama, baba na mtoto na anatarajia kuboresha utaalamu wake katika kutoa huduma za Uzazi wa Mpango kwa wateja baada ya Kujifungua (PPFP).

MARIE STOPES TANZANIA

Plot 421&422 Mwenge, Kijitonyama
P.O. Box 7072.
Dar es Salaam, Tanzania
T: **+255 22 227 4991**
**Toll-Free No. : 0800753333**
E-Mail: info@mst.or.tz

mariestopestz
@MarieStopesTZA
@mariestopestz
marieStopes Tanzania